**Ujinsia na Wajibu wa Binadamu**
**Barua ya Idhini ya Shule ya Msingi**
**Darasa la 2**

Mzazi au Mlezi,
Kwa kuzingatia Sera ya Bodi ya Austin ISD EHAA (Austin ISD Board Policy EHAA), mtaala wa Ujinsia na Wajibu wa Binadamu (Human Sexuality and Responsibility -HSR) utafundishwa msimu huu wa Majani kupukutika (Fall) wakati wa darasa la sayansi la mtoto wako. Masomo 3 katika darasa la 2 yanashughulikia habari ya kukua na inayofaa kwa umri inayohusiana na anatomia, uzazi, na usalama wa kibinafsi. Mtaala huu umeanzishwa ili kutoa habari na ukuzaji ujuzi kwa wanafunzi ili waweze kufikia uwezo wao wa juu zaidi wa afya ya kimwili, kihisia, kiakili na kijamii.

Iwapo bado hujafanya hivyo, tunakualika ukague mtaala mtandaoni at https://www.austinisd.org/pe-health/health-education/hsr (chini ya kitufe cha **K-HS Lessons**). Kama mwalimu mkuu katika maisha ya mtoto wako, AISD inaamini kwamba wewe ndiye chanzo muhimu zaidi cha habari kuhusu ujinsia wa binadamu. Mtaala wa HSR unakusudiwa kusaidia kile ambacho wanafunzi wanajifunza nyumbani, kuheshimu maadili ya familia yako binafsi na kuwafundisha wanafunzi kuheshimu maadili ya familia ya wengine ambayo huenda yakatofautiana na yao wenyewe.

Una haki ya kuamua kama mtoto wako atashiriki katika masomo haya. Ikiwa utachagua mtoto wako asishiriki katika moja au zaidi ya masomo haya, kutakuwa na masomo mbadala, yanayozingatia ujuzi wa kujifunza kijamii na kihisia, inayoandaliwa katika eneo tofauti.

Maelezo yote kuhusu sera ya HSR, muhtasari wa somo kwa kiwango cha darasa, nyenzo za familia, na zaidi yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya HSR: https://www.austinisd.org/pe-health/health-education/hsr. Ikiwa una maswali au wasiwasi wowote, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako au mkuu wa chuo.

***Tafadhali chagua moja ya chaguo zilizo hapa chini, tia sahihi na tarehe, na urudishe fomu hii kwa mwalimu wa mtoto wako.***

KUMBUKA: Ikiwa fomu hii haitarejeshwa, mtoto wako hataweza kushiriki katika masomo yoyote.

☐ **Mtoto wangu atachagua <u>KUINGIA</u> kwa masomo <u>yote</u> 3 ya Ujinsia na Wajibu wa Binadamu.**
*(Ukichagua chaguo hili, umemaliza. Tafadhali ruka hadi chini na utie sahihi na tarehe.)*

**Ninataka mtoto wangu <u>AINGIE</u> kwenye masomo yafuatayo pekee: (chagua yote yanayotumika):**

☐ Somo 1 Mtoto anatengenezwa Vipi (What Makes a Baby)
☐ Somo 2 Mwili Wangu (My Body)
☐ Somo 3 Kuulinda Mwili Wangu (Keeping My Body Safe)

☐ **Mtoto wangu atachagua <u>kutoshiriki</u> katika masomo <u>yote</u> yaliyoorodheshwa hapo juu.**

| ____________________ | ____________________ | __________ |
|---|---|---|
| Jina la Mwanafunzi | Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe |